Swahili Version

BIFAA BYA WAKIMBIZI



# Huduma za mahali unakaa (services communautaires) za Amerika

Wakati unafika Amerika kuna huduma nyingi za mahali unakaa (services communautaires) zenyi unaweza tumikisha. Aina na kadiri ya huduma za mahali unakaa zinapishana kufatana na fasi unaishi. Shirika lako la kuhamishwa (Agence de réinstallation) inaweza kukusaidiya kujuwa na kutumikisha huduma za mahali unakaa alakini na weye unapashwa kujifunza na kuzoweya batu na mahali unaishi ili uweze kujisaidiya peke yako kupata misaada.

## MAFAA YA KUTUMIKISHA HUDUMA ZA MAHALI UNAKAA

Kuelewa watu wa mahali unakaa, na kujuwa huduma gani unaweza tumikisha, itakusaidiya kujuwa kufanya bitu peke yako na kuzoweya inchi. Kwa mfano, huduma fulani zinaweza kukusaidiaya wakati una magumu ya pesa ao magumu fulani kufatana na ulema wa mwili ao wa kichwa. huduma fulani za mahali unakaa zinaweza kukusaidiya kutafuta kazi na kujifunza kingereza. Huduma zingine za mahali unakaa zinasaidiya kushirikiyana na jamaa lako kupitiya michezo ya kujifurahisha. Kukuwa mchangamushi ndani ya communauté yako ni njiya muzuri yenyi itakusaidiya kukutanana na batu bengine na itakusaidiya usikuwe na shida zaidi ya kuzoweya inchi yako ya mupya na mila na tabiya za inchi. Ya mwisho, kuzoweya huduma za mahali unakaa, zaidi services za urgence na police, zitalinda usawa na usalama wako.


## AINA ZA HUDUMA ZA MAHALI UNAKAA

Kuna aina nyingi za huduma za mahali unakaa, zimoja unazipata bila kulipa pesa ao unalipa pesa kidogo. Huduma za mahali unakaa zinaweza tolewa na serkali, ao shirika fulani ndani ya communauté, ao na shirika la dini fulani, ao na wafanya bihashara ya pekee (privé). Kila communauté ina misaada tafauti inapatiya wakaaji. Huduma zenyi unaweza pata hapa amerika ni hizi.

HUDUMA ZA MAHALI UNAKAA (SERVICES COMMUNAUTAIRES) ZA AMERIKA





### Huduma za emergensi na police

Communautés zote zina police, departimenti za kuzimya moto, huduma za emergensi ya afya, na zinatumikiya na zinalinda wakaaji. Ukukutanana na police, ni lazima ubasikilize na usibaogope. Ikiwa hauwezi sumuliya na police juu ya luga, omba bakupe interprète. Kusudi upate msaadsa wa urgence, ita 911 ku simu. Ikiwa hauwezi sumuliya kingereza, unaweza sema "No English. Help" or "No English. Emergency". ("Siseme Kingereza. Muni saidiye" ao "Siseme Kingereza. Mukuye haraka saana.")

### Msaada wa Serkali

Serkali inatoleya huduma nyingi, zimoja zinasaidiya tuu watu ao ma jamaa zenyi kuwa na hiyo haki. Hizo programmes ziko za tafauti nyingi na zinaweza kupatiya watu misaada za chakula, msaada wa pesa, na/ao ukingo wa afya. Programmes za serkali zina tembezwa mara nyingi na agensi za huduma za jamii (service social) za serkali, na watu wanasaidiwa kadiri fulani na kuna kanuni fulani utatimiza mbele usaidiwe.

### Bibliothèques

Bibliothèques za watu wote zina vitabu na byombo bingine, kama CDs na DVDs, ili wkaaji wabikopeshe bila kulipa. Bibliothèque za watu wote, mara nyingi zinatowa programmes zingine, kama michezo za Watoto na masomo za kingereza kwa watu wakubwa. Zinaweza kuwa piya na kompita za watu wote kutumikisha.

### Parcs

Parcs zinafunguliwa kwa watu wote ju ya ma activités za inje, kama kutembeya, kukimbiya, kucheza michezo ao kuikala na kupumuzika. Parcs zimoja zina mahali za pikniki, mahali za kuchezeya, na mahali za kufanya ma sporti. Parcs zina kanuni za kukujulisha nini unaweza fanya na nini hauwezi fanya. Kwa mfano, hauruhusiwe kutupa buchafu chini na karibu parcs zote zinafunga giza ikifika magaribi.

### Ofisi za poste

Unaweza tuma baruwa ao furushi fulani, ao kuuza timbres ku ofisi ya post. Ofisi za Poste za Amerika zinaongozwa na serkali ya inchi.

### Centre za kuburudika ao centres communautaires

Centres za kuburudika ao centres communautaires ni mahali batu banakutananaka ili ba shirikiane mu ma activités fulani ndani ya usawa. Hizo activités zinawezakuwa sports ao michezo, kusoma masomo, ao kushirikiyana na watu wengine mu bitu fulani byenyi kubafaliya. Centres za kuburudika zinapokeya batu bakubwa kama piya batoto, na ma activités unaweza zifanya bila kulipa ao ukilipa.

## AINA YA MSAADA WA SERKALI

Serkali ya inchi inatoleya msaada fulani,na msaada ingine inapewa na serkali ndogo, na piya serkali za muji. Ndiyo maana, haiko programmes zote senyi tunataya hapo chini njo zinapatikana kwa kila mahali. Kuwa na haki ya kusaidiwa na programmes hizo inapishana kufatana na kila mahali, na unaweza azimishwa uwe mwenyi kufanya ma activités fulani na uwe unawatoleya habari zako, kwa mafano kubajulisha kama umebadirisha kazi ao uwezo wako wa pesa umebadirika. Shirirka lako la kuhamishwa litakusaidiya kuitikiwa ku ma programmes zenyi zinaweza kukusaidiya, alakini ni lazima na weye peke yako utajifunza nin utaweza fanya ili wakuitike mwa hizo programmes.

### Programme za msaada wa pesa

Kwa kusaidaya watu wenyi wana shida ya kupata kazi, kuna programmes mbili zenyi kusaidiya na pesa kwa muda mfupi: Shirika la Msaada kwa muda mfupi kuhusu jamaa zenyi kuwa na magumu (TANF) inasaidiya wazazi benyi kuwa na batoto na shirika la Msaada ya Pesa kwa Wakimbizi (RCA) inasaidiya wakimbizi wenyi hawayaowa ao kuolewa na wakimbizi wenyi waliowana alakini hawana Watoto.

### Programme ya kusaidya kipesa watu wenyi kutafuta kazi haraka

Shirika nyingi za kuhamisha watu zinatowa programme hiyo mahali ya msaada wa pesa kwa wakimbizi wenyi kutaka kutumika, alaki wana lazima ya msaada wa pesa kwanza. Wakimbizi wnyi kujiandikisha kwa hio programme wenaitika kufanya nguvu zote zenyi kuwezekana kwa kutafuta kazi. Kwa sababu ya hiyo, wanasaidiwa na pesa, na mashahuri za kutafuta kazi, na wanapewa uwezo wakujifunza kazi ndani ya kampuni mu myezi 4 mpaka 6 kisha kufika hapa Amerika.

### Programme ya kusaidya na pesa ya kuuza chakula (SNAP)

Hiyi ni programme ya inchi inatowa msaada wa pesa kwa watu wenyi kuwa na uwezo ndogo ya pesa za kuishi nazo ili wauze chakula. Mutu mwenyi kuwa ndani ya programme hiyi anapewa kardi yenyi anaweza tumikisha kwa kuuza chakula ya kadiri fulani kila mwezi. Wakimbizi wanaweza omba msaada wa chakula ku ofisi ya serkali ya muji. Utapewa msaada kadiri ya watu wa jamaa lako na uwezo wenu wa pesa. Ikiwa watu ndani ya jamaa lako wameongezeka ama wamepunguka ao uwezo wa pesa umebadirika nyuma ya wewe kupewa msaada wa SNAP, unapashwa julisha mutu mwenyi kushurulikiya hiyo ku ofisi ya serkali y amuji ya fasi unakaa.

### Huduma ya kuongeza usawa wa pesa za kuishi nazo (SSI)

Hili ni programme ya msaada wa pesa unaopewa na serkali ya inchi kwa watu wenyi kuwa vipofu, wapoovu wa mwili, ao watu wenyi kuwa na zaidi ya myaka 65 na wana uwezo wa pesa ndogo za kuishi nazo ao hawana uwezo wowote wa pesa.

### Programmes za kusaidiya kulinda watoto wadogo wa watu wenyi kutumika

Huduma fulani zinatoleya msaada wa kulinda Watoto wadogo wa watu wenyi kutumika kwa beyi ndogo kwa jama zenyi kuwa na uwezo wa pesa ndogo ili wazazi waweze tumika ao waweze tafuta kazi.

Cultural Orientation Resource Exchange
8719 Colesville Road, 3rd Floor • Silver Spring, MD 20910

For more information, visit the CORE Resettlement Navigator website at **corenav.org**.

The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**